

Mualiko

Toa maoni yako juu ya ushiriki wako katika masomo ya Lugha na maandalizi ya ajira (introduksjonsprogrammet!)

Salaam,

Kwa mara ya kwanza washiriki wote wa masomo ya introduksjonsprogrammet wanaalikwa kwenye utafiti wa kitaifa. Ni matumaini yetu kwamba utatumia nafasi hii na utashiriki kutoa maoni yako binafsi.

Utafiti huu unafanywa na idara ya uhamiaji katika kitengo cha ujumuishi wa wananchi wote anuwai kutoka sehemu mbalimbali. (Integrerings- og mangfoldsdirektoratet **IMDi**).

Ili kwamba IMDi na manispaa (Kommune) yako waweze kukupatia huduma bora wewe pamoja na wenzako mnaoshiriki katika masomo, tunahitaji maoni yatokanayo na uzoefu wako. Ni muhimu kwamba majibu ya maswali haya yatolewe kwa uwazi na kwa uaminifu, ili tuweze kupata maelezo yatakayotuongoza kuboresha mambo yanayopaswa kufanyiwa marekebisho. Kwa mfano, utaulizwa ikiwa umeridhika na masomo unayoshiriki sasa, unayafurahia ama kuna kitu ambacho hakiko sawa katika programu unayoshiriki.

Utafiti huu ni wa hiyari yako na itachukua takriban dakika 30 kujibu maswali utakayoulizwa.

Utafiti unafanywa bila wewe kuandika utambulisho wako. Majibu utakayotoa hayawezi kufuatiliwa ili kutambua kuwa wewe ndiwe uliyetoa majibu kwa maswali utakayoulizwa. Maelezo yote utakayotoa yatatunzwa kwa siri na watumishi wa IMDi na watafiti wachache walioteuliwa wenye uwezo wa kuona utafiti huu. Hakuna wafanyakazi wa manispaa (Kommune) watakaoruhusiwa kuona majibu yako binafsi.

Ikiwa una maswali kuhusu utafiti au matatizo ya kiufundi basi wasiliana na IMDi kwa barua pepe: post@imdi.no Tambulisha barua yako kwa neno: **Brukerundersøkelse**.

Manispaa yako inakuwezesha kujiunga na utafiti huu.

Asante kwa ushirikiano wako wa kuiboresha programu ya masomo ya lugha na maandalizi ya ajira. (introduksjonsprogrammet)

Wasalaam,

Integrerings- og mangfoldsdirektoratet



post@imdi.no
www.imdi.no

*Msingi wa kushughulikia utafiti huu umejengwa juu ya ridhaa ya mshiriki wa utafiti huu.
Maswali yoyote juu ya ulinzi wa faragha ya mshiriki wa utafiti huu yanaweza kutumwa kwa
Karianne Thun kth@imdi.no*

*Ikiwa kutakuwa na malalamiko kwa IMDi juu ya uvunjifu wa faragha ya mtu na kusambaza
maelezo binafsi yahusianayo na utafiti huu waweza kuwasiliana na **Datatilsynet**. Maelezo zaidi
yanapatikana kwenye tovuti ya *Datatilsynet*.*